



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI (AFISI YA RAIS) KATIBA NA UTAWALA BORA,  
MHESHIMIWA RAMADHAN ABDALLA SHAABAN (MBM) KATIKA BARAZA LA  
WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA  
FEDHA 2009/2010**

**JULAI, 2009**

## YALIYOMO

UTANGULIZI.....	1
MUHTASARI WA UTEKELEZAJI.....	2
UTEKELEZAJI KIFEDHA.....	3
IDARA YA MIPANGO NA SERA .....	4
MAHAKAMA .....	6
AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI.....	8
AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA .....	11
AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI .....	13
AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR .....	16
IDARA YA URATIBU UTAWALA BORA .....	18
AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI .....	21
AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI .....	23
KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA.....	26
AFISI KUU PEMBA.....	28
CHANGAMOTO .....	30
SHUKURANI.....	30
HITIMISHO .....	31
KIAMBATISHO 1: FEDHA ZILIZOINGIZWA KWA MATUMIZI YA KAWAIDA.....	32
KIAMBATISHO 2: FEDHA ZA MIRADI .....	33
KIAMBATISHO 3: MAKUSANYO YA MAPATO (2008/2009) NA MAKADIRIO YA 2009/2010 ...	34
KIAMBATISHO 4: MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO 2009/2010.....	35
KIAMBATISHO 5: MIRADI YA MAENDELEO 2009 - 2010.....	36
KIAMBATISHO NAMBA 6a: IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO YA MUDA MREFU 2008/2009.....	37

<b>KIAMBATISHO NAMBA 6B: IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO YA MUDA MFUPI 2008/2009 .....</b>	<b>38</b>
<b>KIAMBATISHO NAMBA 7a:UFUNGUAJI WA KESI KATIKA MAHAKAMA MBALIMBALI JULAI 2008 HADI MACHI 2009.....</b>	<b>39</b>
<b>KIAMBATISHO 7b: UFUNGUAJI WA KESI KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO.....</b>	<b>41</b>
<b>KIAMBATISHO 7c: UFUNGUAJI WA KESI KATIKA MAHAKAMA ZA KADHI WA WILAYA .....</b>	<b>41</b>
<b>KIAMBATISHO NAMBA 8: KESI ZILIZOFUNGULIWA NA KUSIMAMIWA NA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA JULAI 2008 HADI MACHI 2009 .....</b>	<b>42</b>
<b>KIAMBATISHO NAMBA 9a: VIZAZI NA VIFO VILIVYOSAJILIWA KIWILAYA .....</b>	<b>43</b>
<b>KIAMBATISHO NAMBA 9b: NYARAKA ZILIZOSAJILIWA.....</b>	<b>44</b>
<b>Kiambatisho Nam. 10a : Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji 2008.....</b>	<b>45</b>
<b>Kiambatisho Nam 10b: Jumuiya zilizombewa Msamaha wa Ushuru .....</b>	<b>46</b>
<b>KIAMBATISHO 11a: MISWADA ILIYOANDALIWA NA AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: .....</b>	<b>46</b>
<b>KIAMBATISHO 11b: KANUNI ZA AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:.....</b>	<b>47</b>
<b>Kiambatisho 12 a: Idadi ya wafanyakazi wa Wizara.....</b>	<b>48</b>
<b>Kiambatisho 12b: Idadi ya wafanyakazi Unguja na Pemba .....</b>	<b>49</b>
<b>Kiambatisho 12c: Ajira Mpya.....</b>	<b>50</b>

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI (AFISI YA RAIS) KATIBA NA UTAWALA BORA,  
MHESHIMIWA RAMADHAN ABDALLA SHAABAN KATIKA BARAZA LA  
WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA  
NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2009/2010**

**UTANGULIZI**

- 1. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi (Afisi ya Rais) Katiba na Utawala Bora kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.
- 2. Mheshimiwa Spika,** kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya na kuweza kufika tena hapa leo hii kuendelea na shughuli yetu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie hikma, busara na atupe muelekeo mwema na mashirikiano zaidi ili tuweze kufanikisha jukumu letu vizuri.
- 3. Mheshimiwa Spika,** baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume kwa juhudi zake mbali mbali za kuimarisha uchumi. Aidha nampongeza kwa kuwa mstari wa mbele katika kuilinda amani, kudumisha utulivu uliopo na kupambana na janga la umasikini.
- 4. Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii pia kumpongeza Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, utendaji mzuri na usimamizi wa siku hadi siku wa shughuli za Serikali. Vilevile napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliendesha vyema Baraza letu hili Tukufu.
- 5. Mheshimiwa Spika,** aidha, naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza wajumbe wako wote kwa kusaidia kutoa maelekezo kwa Wizara yangu ili kuona kuwa lengo la kuimarisha Utawala Bora linatimia. Nawapongeza na kuwashukuru sana wajumbe walioichangia hotuba ya Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2008/2009. Pongezi za pekee nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako Tukufu

chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Haji Omar Kheri, kwa ushauri, maelekezo na busara zao kwa wakati wote. Hakika michango yao imekuwa chachu kwa Wizara yangu katika kutekeleza vyema majukumu yake.

- 6. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa nitaeleza kwa muhtasari hali halisi ya utekelezaji wa majukumu ya kazi mbalimbali za Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2008/2009.

#### **MUHTASARI WA UTEKELEZAJI**

- 7. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia taasisi zake mbalimbali imeweza kutekeleza sehemu ya malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kama ifuatavyo:

- i. Kesi zisizo za uhakika zimepunguzwa kwa kiasi kikubwa kutokana na utaratibu wa kukamilisha upelelezi kabla ya kupeleka kesi Mahakamani.
- ii. Kukamilika utayarishaji na uandishi wa ripoti ya mwaka 2007/2008 ya ukaguzi wa hesabu za Serikali na kuendelea na ukaguzi wa hesabu za mwaka 2008/2009.
- iii. Kushiriki hatua mbalimbali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujitathmini kuhusu Utawala Bora kupitia mpango wa nchi za Afrika kujitathmini wenyewe (APRM).
- iv. Kuchapisha nakala za sheria za Zanzibar kutoka mwaka 1980 hadi 2007 na kusambazwa kwa watumiaji mbalimbali serikalini, taasisi za sheria, maktaba kuu, vyo vya elimu na kwa Wanasheria wa Serikali.
- v. Kuanza kufanyakazi kwa Kamati ya pamoja ya kuharakisha usikilizaji wa kesi na kutolewa maamuzi.
- vi. Kufanya ukarabati mdogo katika majengo ya Mahakama za Wilaya Mwanakwerekwe, Chake Chake, na ujenzi wa Mahakama ya Mwera unaendelea vizuri.
- vii. Kuanza kazi kwa Afisi ya Msajili wa Hakimiliki huko Pemba.

- viii. Kukamilika kwa ukarabati katika chumba maalum cha kuhifadhia nyaraka katika jengo la Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na kuendeleza kazi za ujenzi wa jengo la Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali Pemba kwa kuliezekwa.
- ix. Ujazaji wa mikataba mipya ya upangaji wa nyumba zilizo chini ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ili kukidhi matakwa ya sheria mpya ya Kamisheni ambapo hadi sasa kazi hiyo inakaribia asilimia 50.
- x. Kuwasomesha wafanyakazi 165, kati ya hao 61 mafunzo ya muda mrefu na 104 mafunzo ya muda mfupi katika ngazi mbalimbali. **(Angalia kiambatisho namba 6a na 6b).**
- xi. Kuzinduliwa kwa Mwongozo wa Haki za Binaadamu kwa mujibu wa sura ya tatu ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.
- xii. Kupitishwa na kusambazwa kwa wadau mbali mbali Sera ya Jumuiya zisizo za Kiserikali.

#### **UTEKELEZAJI KIFEDHA**

- 8. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya Tsh.. 4,583,852,000.00 ambapo hadi mwezi Machi, 2009 fedha zilizopatikana ni Tsh. 3,092,615,985 sawa na asilimia 67%. Kati ya hizo Tsh.1,698,493,849 sawa na asilimia 73 kwa mishahara na maposho na Tsh. 1,394,122,136 sawa na asilimia 62 kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa kazi za maendeleo, fedha zilizoidhinishwa ni Tsh. 803,000,000.00, hadi kufikia Machi, 2009 fedha zilizopatikana ni Tsh. 585,000,000.00 sawa na asilimia 73 ya makadirio.
- 9. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa washirika wa maendeleo fedha zilizokadiriwa ni Tsh. 1,160,862,346 ambapo hadi kufikia Machi, 2009 fedha zilizopatikana ni Tsh. 573,677,021 sawa na asilimia 49 ya makadirio. Wizara pia inakusanya mapato kupitia Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, Mahakama na Afisi ya Mdhimiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Makadirio yalikuwa ni Tsh. 292,928,000.00 na hadi kufikia Machi, 2009 fedha zilizokusanywa Tsh. 198,326,422.00 sawa na asilimia 68 ya

makadirio. Matarajio ni kukusanya Tsh. 264,435,229.00 ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni sawa na asilimia 90. **(Angalia kiambatanisho Nam 1, 2 na, 3)**. Maelezo zaidi ya utekelezaji wa kazi za kawaida na malengo kupitia Idara na Taasisi za Wizara kwa mwaka 2008/2009 ni kama ifuatavyo:-

## **IDARA YA MIPANGO NA SERA**

**10. Mheshimiwa Spika**, Idara hii ndio yenye jukumu kubwa la kuratibu shughuli za Wizara. Hadi kufikia Machi, 2009 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

### **Kuimarisha uwezo wa Idara katika kuratibu shughuli na kazi za Wizara**

**11. Mheshimiwa Spika**, Idara ya Mipango na Sera imeendelea kuratibu kazi zake baina ya Wizara na Wizara nyengine kwa kutayarisha taarifa za utekelezaji wa Miradi kwa kila mwezi na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Uchumi; na taarifa za utekelezaji llani ya uchaguzi ya CCM. Idara pia imeshiriki kazi mbalimbali za kitaifa kama vile utayarishaji wa Ripoti ya Mwaka Mmoja ya Utekelezaji MKUZA; mapitio ya mpango mkakati wa kupiga vita UKIMWI; na mapitio ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya MKUZA. Idara pia imekuwa ikipokea nyaraka mbalimbali kwa ajili ya rejea na kuzihifadhi katika Kitengo cha Mipango. Aidha, taarifa mbalimbali zinaendelea kukusanywa kwa ajili ya kuingizwa kwenye tovuti ya Wizara ambapo anuani yake ni [www.kubzanzibar.org](http://www.kubzanzibar.org).

**12. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa Idara kwa kuwapeleka wafanyakazi saba masomoni, kati ya hao sita wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na mmoja ya muda mfupi. **(Angalia kiambatanisho 6a na 6b)**. Watendaji wa Wizara wamehudhuria semina za kazi zikiwemo uingizaji wa masuala ya kijinsia katika sera na mipango ya Serikali na ufuatiliaji wa matumizi ya bajeti (Budget Tracking). Aidha, Wizara imeshiriki hatua mbalimbali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujitathmini kuhusu Utawala Bora kupitia mpango wa nchi za Afrika kujitathmini wenyewe (African Peer Review Mechanism - APRM). Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ripoti ya Kitaifa yenye mpango-kazi wa utekelezaji.

**13. Mheshimiwa Spika,** idara imeendelea kuratibu mpango wa manunuzi wa Wizara ambapo hadi Machi, 2009 vikao saba (7) vya Bodi ya Zabuni vimefanyika. Miongoni mwa kazi kubwa zilizofanywa na Bodi ni kukamilisha mchakato wa kumpata mtaalamu muelekezi wa kufanya mapitio ya sheria zinazosimamia biashara 'Business Entry, Exist and Security Registration' zilizo chini ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Napenda kuliarifu Baraza lako kuwa mikataba kwa ajili ya kazi hii kati ya Wizara na Kampuni ya 'Norway Registry Development' imeshafungwa na kwamba kazi hiyo imeshaanza.

#### **Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI**

**14. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea na mapambano dhidi ya UKIMWI yaliandaliwa mafunzo kwa Jumuiya mbili zisizo za Serikali zinazojihusisha na masuala ya kisheria hapa Zanzibar (Chama cha wanasheria wanawake na Kituo cha huduma za sheria Zanzibar). Lengo kuu ni kuangalia kwa namna gani waathirika wa UKIMWI wanaweza kupata msaada wa kisheria na pia kutafuta njia nzuri ya kulinda haki zao kisheria. Idara pia iliendesha mafunzo kwa wajumbe wa kamati ya UKIMWI ya Wizara Unguja na Pemba na kuendesha zoezi maalum la upimaji wa damu kwa hiari kwa wafanyakazi wa Wizara na familia zao ambapo katika zoezi hilo lililoongozwa na Katibu Mkuu watu 50 walichunguzwa afya zao na kukutikana salama. Idara pia iliandaa mafunzo ya siku moja (1) yaliyowajumuisha watoto wa wafanyakazi. Aidha vipindi vinne (4) vya redio vinavyohusiana na uelimishaji umma juu ya haki za watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI pamoja na unyanyapaa vilirushwa hewani.

#### **Kuendelea na kazi ya kulifanyia matengenezo jengo la Wizara**

**15. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango na sera kwa mwaka 2008/2009 imeweza kufanya ukarabati wa mfumo wa mawasiliano wa ndani na pia kuzifanyia ukarabati sehemu mbalimbali za jengo.

#### **Kutekeleza na Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa Kimkakati wa Wizara**

**16. Mheshimiwa Spika,** katika kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Kimkakati wa Wizara, Idara ya Mipango na Sera imeitisha vikao vya kila mwezi kwa

ajili ya kuutekeleza mpango wa Kimkakati hasa wakati wa utayarishaji wa Mpango wa Mwaka, "Medium Term Expenditure Framework" (MTEF) na utekelezaji wa Mipango ya idara/taasisi iliyojipangia.

**17. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka fedha wa 2009/2010, idara ya Mipango na Sera imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Kuimarisha uwezo wa Idara katika kuratibu shughuli na kazi za Wizara
- b) Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI

**18. Mheshimiwa Spika,** ili Idara ya Mipango na Sera iweze kutekeleza malengo hayo kwa mwaka 2009/2010, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh. 470,967,000.00 kwa kazi za kawaida.

## **MAHAKAMA**

**19. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi 2008/2009, jumla ya kesi 4,236 zilifunguliwa ambapo kesi 1,234 ni za madai na 2,762 ni za jinai. Aidha rufaa za madai 157 na rufaa za jinai 83 zilifunguliwa (**Angalia kiambatanisho 7a na 7b**). Kati ya kesi 4,236 zilizofunguliwa, kesi 2,156 zimetolewa uamuzi ambapo ni sawa na asilimia 50.7. Hadi kufikia Machi, 2009 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

### **Matengenezo ya jengo la Mahakama Kuu Vuga**

**20. Mheshimiwa Spika,** matengenezo ya jengo hili hayakuweza kufanyika kutokana na kutegemea fedha za wafadhili ambazo hazikupatikana. Katika mwaka ujao wa fedha Serikali imeshatenga jumla ya Tsh. 550,000,000.00 kuhakikisha matengenezo hayo yanafanyika.

### **Tathmini ya Mpango wa Wahalifu kutumikia jamii**

**21. Mheshimiwa Spika,** Mahakama imeendelea kufanya tathmini ya mpango wa wahalifu kutumikia jamii kwa kufanya vikao na Mahakimu na wadau wengine ili kuweka mikakati muafaka. Mpango huu unakabiliwa na vikwazo vinavyochangia kutoendelea vizuri ikiwa ni pamoja na upungufu mkubwa wa "Probation Officers" kutoka Idara ya Ustawi wa Jamii ambapo kwa sasa idadi ya maafisa waliopo ni wawili tu.

Vikwazo vyengine ni pamoja na uelewa mdogo wa jamii, na kukosekana kwa ridhaa ya wahalifu kutumikia adhabu hiyo kama kanuni inavyoelekeza. Hata hivyo Mahakama inaendelea kuchukua juhudi za kuwasiliana na Idara husika ili kuweza kuwapata "Probation Officers" kwa lengo zima la kurahisisha mpango huo.

**Kuanzisha Kamati ya kusukuma kesi.**

**22. Mheshimiwa Spika,** Mahakama imeanzisha Kamati ya kusukuma kesi kwa lengo la kuharakisha utoaji wa maamuzi. Kamati hii inajumuisha wadau mbalimbali wakiwemo Mahakimu, Wanasheria kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Polisi, Jeshi la Mafunzo, Mkemia Mkuu na Madaktari. Kamati hii imeshakutana mara tatu na mafanikio yameanza kuonekana katika kupungua kwa ucheleweshaji wa kufanyika upelelezi, usikilizaji wa kesi na utoaji wa maamuzi, mambo ambayo yatapelekea kupungua kwa mrundikano wa kesi na mahabusu, na malalamiko ya wananchi dhidi ya vyombo vya sheria.

**Kujenga jengo jipya la Mahakama Tunguu na kukarabati majengo ya zamani.**

**23. Mheshimiwa Spika,** kazi ya ujenzi wa jengo jipya la Mahakama ya Mkoa Tunguu haikuanza kama ilivyopangwa kutokana na uhaba wa fedha zilizopatikana. Hata hivyo, fedha zilizopatikana ilionekana ni bora zitumike kwa ujenzi wa Mahakama ya Mwera ambayo inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2009.

**24. Mheshimiwa Spika,** matengenezo madogo madogo yameendelea ambapo Mahakama za Mwanakwerekwe, Makunduchi na Mfenesini zimekarabatiwa. Mahakama pia imepatiwa jengo lililokuwa la Maktaba Kuu liliopo pembezoni mwa Mahakama Kuu Vuga. Jengo hilo litatumika kwa kazi za Mahakama mara tu matengenezo yanayoendelea yatakapokamilika.

**25. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji na kujenga uwezo zaidi wa watumishi, Mahakama imewapeleka wafanyakazi wake wanane wa kada mbali mbali masomoni. Wafanyakazi hao wanne wanaume na wane wanawake. **(Angalia Kiambatanisho 6a na 6b).** Aidha, Mahakama

imeweza kununua vitendea kazi mbali mbali na kusambazwa katika Mahakama zake za Unguja na Pemba vikiwemo kompyuta, samani, gari mbili (2) na jenereta moja (1).

**26. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2009/2010 Mahakama imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

- a) Kuimarisha uwezo wa Mahakama kwa kuwaongezea taaluma watendaji na kuimarisha upatikanaji wa vitendea kazi.
- b) Kufanya matengenezo ya jengo la Mahakama Kuu Vuga.
- c) Kuimarisha kamati ya kusukuma kesi
- d) Kuimarisha mpango wa wahalifu kutumikia jamii

**27. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Mahakama ilikadiria kukusanya na kuchangia katika Hazina ya Serikali jumla ya Tsh. 41,200,000.00 ambapo hadi kufikia Machi, 2009 fedha zilizokusanywa ni Tsh. 25,937,814.00 sawa na asilimia 62 ya makadirio. Makusanyo haya yalitarajiwa kufikia Tsh. 34,583,752.00 hadi kufikia mwezi Juni, 2009.

**28. Mheshimiwa Spika,** Mahakama ili iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka 2009/2010 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh. 1,298,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Tsh. 550,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha Mahakama katika mwaka 2009/2010 inakusudia kuchangia katika Hazina ya Serikali mapato ya Tsh. 42,000,000.00.

#### **AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

**29. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliendelea na Utekelezaji wa Majukumu yake ya kuwa Mshauri Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo yote ya kisheria. Aidha Afisi iliendelea na utekelezaji wa kazi za kawaida na kukamilisha malengo iliyojiwekea.

**30. Mheshimiwa Spika,** Afisi ilipata Ufadhili kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP) wa jumla ya Tsh. 235,691,346.00 kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi, ununuzi wa vifaa vya afisi, uchapaji wa sheria kutoka 1980-2007, kuwapatia semina Wanasheria wa Serikali pamoja na maafisa

wengine wa sheria na kada tofauti kutoka Wizara na taasisi mbali mbali za Serikali na binafsi.

**31. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Afisi imeweza kuwapatia semina wanasheria wake wote katika fani ya Dhana juu ya Rushwa, Dhana juu ya Usafirishaji Fedha Haramu na madhara yake kwa taifa, Dhana juu ya Ugaidi na hasara zake kwa jamii. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi, wafanyakazi wanane walipata mafunzo ya fani mbali mbali yakiwemo; "Financial Management in Donor Fund", "Performance Auditing", "Performance Appraisal" na "Legal Drafting". Aidha, wafanyakazi watano wamepelekwa katika mafunzo ya muda mrefu ambao mwanamme mmoja (1) na wanawake wanne (4). Sambamba na hilo, Afisi pia imeweza kutoa mafunzo ya vitendo (Internship) kwa Wanasheria kumi (10) wa Serikali kutoka Mawizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2008/2009. **(Angalia Kiambatanisho 6a na 6b).**

**32. Mheshimiwa Spika**, vitabu mbalimbali vya sheria na majarida yamepatikana na kuwapa fursa wanasheria kuvitumia kwa shughuli zao za kila siku katika Maktaba mpya ya Afisi. Aidha, Afisi imeimarisha mfumo wake wa kimawasiliano kupitia 'satellite dish' ili kuenda sambamba na mabadiliko ya ulimwengu na kuona kupitia televisheni matukio yanayotokea na maamuzi yanayochukuliwa na vyombo vyengine vya sheria duniani zikiwemo Mahkama za Afrika Mashariki, Mahakama ya kivita iliyoko The Hague Uholanzi, n.k.

### **Kuimarisha kazi za uchapishaji wa Sheria za 2007 na 2008 pamoja na Sheria ndogo ndogo (subsidiary Legislations) za 1980-2008**

**33. Mheshimiwa Spika**, Afisi imeweza kukamilisha uchapishaji wa sheria za mwaka 1980-2007 na tayari zimeshasambazwa kwa wadau wa sheria, kwa upande wa sheria za mwaka 2008 bado zipo kiwandani kwa kuchapishwa na zinatarajiwa kutoka pamoja na sheria ndogondogo (Subsidiary Legislations) za 1980-2008. Aidha Afisi imeweza kutengeneza Miswada tisa (9) ya sheria na kanuni mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2008/2009. **(Angalia Kiambatanisho 11a na 11b)**

**34. Mheshimiwa Spika,** lengo la uchapishaji wa vitabu vya Sheria za Zanzibar limeendelea kutekelezwa kwa kukusanya Sheria hizo za kuanzia mwaka 1964 hadi mwaka 1979 na Sheria za Mwaka 1980 hadi mwaka 2008 ili kuweka kumbukumbu za sheria zilizo sahihi. Kwa hivi sasa nakala za sheria za Zanzibar za kati ya mwaka 1980 na 2007 zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau wa sheria. Sheria za mwaka 2008 zipo kwa mchapishaji na hivi karibuni zitatoka pamoja na sheria ndogo ndogo (subsidiary legislations) za 1980 - 2008.

**Kuendelea na uimarishaji wa Tume ya Kuchunguza Sheria pamoja na utendaji wa kazi zake**

**35. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kuchunguza Sheria inaendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vifaa mbali mbali vya matumizi ya Afisi. Hata hivyo miongoni mwa matatizo yanayoikabili Tume hiyo ni ukosefu wa Mwenyekiti, Makamishna pamoja na wafanyakazi wengine. Hatua za uteuzi wa Mwenyekiti na Makamishna zinaendelea.

**Kuanza matayarisho ya ujenzi wa Jengo jipya la Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.**

**36. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia sasa afisi imefanikiwa kupata kiwanja cha ujenzi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba na kazi ya ujenzi wa uzio inaendelea pamoja na kumtafuta Mshauri muelekezi wa ujenzi.

**37. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2009/2010 Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi kwa kuwawezesha wafanyakazi kitaaluma.
- b) Kuendelea kuchapisha sheria za Zanzibar kutoka mwaka 1964-1979 na kutoka mwaka 1980 – 2009, pamoja na sheria ndogo ndogo.
- c) Kuendelea kuimarisha Tume ya Kuchunguza Sheria na Kufanya mapitio ya sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho yanayostahiki kwa mujibu wa hali iliyopo sasa.
- d) Kuendelea na ujenzi wa majengo mapya Unguja na Pemba.

**38. Mheshimiwa Spika**, ili Afisi ya Mwanasheria Mkuu iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2009/2010 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe Tsh. 546,076,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida na kiasi cha Tsh. 140,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

#### **AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**

**39. Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa la Afisi hii ni kusimamia kesi katika Mahakama mbali mbali za Zanzibar.

**40. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza kazi zake za kawaida, Afisi ilifungua na kusimamia jumla ya kesi 778 katika Mahakama mbali mbali. Mahakama ya Rufaa Tanzania kesi 4, Mahakama Kuu ya Vuga kesi 92, Mahakama Kuu Pemba kesi 19, Mahakama ya Mkoa Mjini Magharibi – Vuga kesi 94, Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja iliyopo Mwera kesi 99, Mahakama ya Mkoa Kaskazini Unguja iliyopo Mfenesini kesi 73, Mahakama ya Mkoa kaskazini Pemba iliyopo Wete kesi 23, Mahakama ya Mkoa Kusini Pemba iliyopo Chake kesi 38 na Mahakama za Wilaya ya Mjini na Magharibi zilizopo Mwanakwerekwe kesi 336. **(Angalia kiambatisho namba 8)**

**41. Mheshimiwa Spika**, Afisi ilipokea majalada 153 ya malalamiko mbali mbali yakiwemo malalamiko juu ya kesi za kubaka, kutorosha wasichana walio chini ya uangalifu wa wazazi wao nk. Majalada hayo yameshapatiwa ufumbuzi na kurejeshwa Polisi.

**42. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2009 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

#### ***Kuimarisha uwezo wa utendaji wa Afisi***

**43. Mheshimiwa Spika**, Afisi iliwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 8, sita katika ngazi ya Shahada ya Uzamiliya Sheria, mmoja Shahada ya Kwanza ya uongozi wa Biashara na mwengine alijiunga na Stashahada ya Sheria. Afisi pia ilifanikiwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 8, kati ya hao 7 wamepatiwafunzo ya Uendeshaji wa Mashtaka - Tanzania Bara, na mmoja amepatiwafunzo ya Utunzaji wa Kumbukumbu huko Arusha. Kadhalika, Afisi iliandaa mafunzo ya

kitaalamu (forensic evidence) kwa wanasheria wake wote na baadhi ya mahakimu wa Mikoa. (**Angalia Kimbatanisho Nam. 6a na 6b**).

**44. Mheshimiwa Spika,** Afisi ilikusanya taarifa zake muhimu ambazo zitaingizwa katika tovuti yake ya Afisi. Uzinduzi wa tovuti hiyo utafanyika mwanzoni mwa mwaka huu wa fedha. Aidha, kwa upande wa majengo, Afisi imekamilisha hatua ya kuezeka ghorofa ya kwanza katika jengo jipya la Makao Makuu ya Afisi.

***Kuimarisha mfumo wa uendeshaji wa mashtaka kwa kujenga utaratibu wa kukamilishwa upelelezi kabla ya kufungua mashtaka***

**45. Mheshimiwa Spika,** Afisi ilifanikiwa kuendeleza azma yake ya kukamilisha upelelezi kabla ya kufungua kesi. Mfumo huo umewezesha kwa kiasi kikubwa kupunguza mrundikano wa kesi ambazo zingepolekwa mahakamani bila ya kuwa na ushahidi wa kutosha. Katika mwaka huu wa fedha, Afisi ilikubaliana na Jeshi la Polisi kutumia utaratibu huo wa kesi kwa kesi za mauaji na ajali za barabarani.

***Kuandaa mapendekezo ya mpango wa pamoja wa usimamizi wa jinai (Zanzibar Criminal Justice Framework)***

**46. Mheshimiwa Spika,** Afisi ilifanya mkutano na wadau kadhaa wanaoshughulikia makosa ya Jinai na kupokea mapendekezo ya mpango wa pamoja wa usimamizi wa Makosa hayo (Zanzibar Criminal Justice Framework), mapendekezo hayo yameshawasilishwa katika taasisi nyengine zinazohusika kwa hatua zaidi.

**47. Mheshimiwa Spika,** Afisi pia imepokea mapendekezo ya marekebisho ya mapitio ya Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sheria ya Mwenendo wa makosa ya Jinai na Sheria ya Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mkutano wa wadau wa kujadili rasimu ya mswada wa sheria ya Zanzibar ya Kupambana na Fedha Haramu pia ulifanyika, rasimu hiyo imepitishwa na inaendelea na hatua nyengine ili kuifanya kuwa sheria rasmi. Aidha, Afisi imefanya mikutano iliyowashirikisha Masheha wa Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi ili kuwafahamisha taratibu za

msingi za uendeshaji wa Mashtaka ya Jinai na mchango wao unaohitajika katika kuboresha uendeshaji wa Mashtaka hayo.

**Kukamilisha na kuimarisha hatua ya tatu ya mpango wa uendeshaji mashtaka katika ngazi ya wilaya (*Third Phase of the Roll out to civilization*)**

**48. Mheshimiwa Spika,** Katika kufanikisha azma ya hatua ya tatu ya mpango wa uendeshaji wa Mashtaka katika ngazi ya Wilaya, Afisi imeweza kupata jengo la Afisi Mwanakwerekwe kwa ajili ya kitengo cha mashtaka kwa Mahakama za Wilaya na hatua za kulitengeneza zimeanza kufanyika.

**49. Mheshimiwa Spika:** Afisi inaendelea na uimarishaji wa huduma za maktaba ambapo inatarajia kupata vifaa kwa ajili ya maktaba mpya vyenye thamani ya Dola za Kimarekani 360,000.00 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB). Maktaba mpya na ya kisasa ya Afisi inatarajiwa kuzinduliwa rasmi Julai, 11 mwaka huu.

**50. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010. Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeazimia kutekeleza yafuatayo:-

- a. Kuimarisha uwezo wa utendaji wa Afisi.
- b. Kuanza utekelezaji mpango wa pamoja wa usimamizi wa kesi za jinai.
- c. Kuimarisha Maktaba na kufanya kituo cha mafunzo na utafiti wa sheria.
- d. Kukamilisha sheria ya kuanzishwa Afisi na kurekebisha Muundo wa Afisi kulingana na sheria mpya.

**51. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itekeleze majukumu yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh.653,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Tsh. 300,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

**AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**52. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni taasisi iliyopewa mamlaka ya juu kisheria kufanya ukaguzi wa mahesabu katika taasisi mbalimbali za Serikali.

**53. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Afisi imekamilisha ripoti ya ukaguzi wa hesabu ya mwaka 2007/2008. Aidha ukaguzi wa hesabu za mwaka 2008/2009 unaendelea vizuri na unatarajiwa kukamilika kwa wakati na kutoa ripoti kwa mujibu wa sheria. Kwa upande wa kazi za ukaguzi wa hesabu za viinua mgongo hadi kufikia Machi, 2009, Afisi imepokea majalada 1,205 ya wastaafu kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi ambapo majalada 1,168 yamekaguliwa. Aidha majalada 612 ya wastaafu yamepokelewa ambapo majalada 600 yamekaguliwa. Hali hii inaashiria kwamba Afisi imeweza kuondoa usumbufu mkubwa wa urundikanaji wa majalada kwa wastaafu.

**54. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2009 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

**Kufanya ukaguzi katika taasisi za Serikali pamoja na miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo.**

**55. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Afisi imeweza kuendelea kufanya ukaguzi katika taasisi zote za Serikali, miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo pamoja na Halmashauri za Wilaya. Aidha Afisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeendelea kutoa ushauri wa kitaalam kwa watendaji wa Halmashauri za Wilaya juu ya uwekaji wa kumbukumbu mbali mbali kwa kufuata sheria na taratibu za hesabu.

**Kuendeleza mashirikiano baina ya Afisi ya Mdhhibiti Mkuu wa Serikali na Afisi nyengine za ukaguzi na Washirika wa Maendeleo.**

**56. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2008/2009, Afisi imeendeleza mashirikiano na Afisi nyengine za ukaguzi duniani kama vile Afisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu Tanzania, Uganda, Sweden n.k pamoja na Washirika wa Maendeleo wakiwemo," WORLD BANK na ADB". Kupitia ushirikiano huo, Afisi imeendelea kufaidika kwa kupatiwa mafunzo na vitendea kazi.

**57. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mashirikiano na Afisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu Tanzania, afisi imeweza kufanya ukaguzi wa pamoja katika taasisi za miradi ya MACEMP, PADEP, Malaria, mradi wa UKIMWI

na miradi mingine inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo. Aidha, Afisi imepeleka wafanyakazi wawili (2) kushiriki mafunzo ya muda mfupi katika taaluma ya juu ya uhasibu na kushirikiana katika kuiwakilisha Tanzania katika mikutano mbali mbali ya kimataifa.

**Kujenga uwezo wa Afisi Kiutendaji na Vitendea Kazi.**

**58. Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanikiwa kupata kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Afisi huko Pemba, Aidha Afisi imekodi jengo kwa ajili ya afisi za makao makuu zilizopo Maisara Unguja. Afisi pia imeweza kupata msaada wa samani, kompyuta, printa na fotokopi kutoka Afisi ya Ukaguzi ya Sweden na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Vile vile Afisi imeweza kujiimarisha kwa kupata vitendea kazi, zikiwemo vespa ishirini (20) na basi moja kupitia Serikali na mradi wa 'Public Financial Management Reform Program' (PFMRP).

**59. Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanikiwa kuwasomesha wafanyakazi wake mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi. Jumla ya wafanyakazi kumi na tisa (19), wanawake wanane (8) na wanaume kumi na moja (11) wanaendelea na masomo katika vyuo mbalimbali. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi, wafanyakazi thelathini na tisa (39) wanawake kumi na tano (15) na wanaume ishirini na nne (24) wamepatiwa mafunzo maalumu ya kiingereza katika taasisi ya RUSCENTRE Zanzibar. Aidha mfanyakazi mmoja (1) mwanamme amepatiwa mafunzo ya kompyuta nchini India na wafanyakazi sita (6) mwanamke mmoja (1) na wanaume watano (5) wamepatiwa mafunzo ya "Viongozi wa Mabadiliko" (leaders of change) yaliyotolewa na taasisi ya Tanzania Global Development Learning Centre. (**Angalia kiambatanisho 6a na 6b**). Aidha, katika kujiimarisha kiutendaji Afisi imeajiri wafanyakazi wapya kumi (10).

**Kujenga uwezo na uhusiano mzuri na wadau mbali mbali ikiwemo PAC na Taasisi nyenginezo.**

**60. Mheshimiwa Spika,** Afisi imeweza kuwapatia mafunzo maalum ya kujenga uwezo juu uelewa wa sheria na kanuni za fedha wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi wa Hesabu na Kamati ya Fedha na Uchumi za

Baraza la Wawakilishi. Aidha Afisi imeweza kuandaa kongamano la wadau wake kutoka taasisi mbali mbali, kwa ajili ya kujadili rasimu ya mradi wa kuimarisha utendaji wa Afisi unaofadhiliwa na Afisi ya ukaguzi wa hesabu Sweden.

**61. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- b. Kuongeza Uwezo wa Watendaji, Vitendea Kazi na Mazingira ya Afisi.
- c. Kufanya Ukaguzi wa Hesabu kwa kuzingatia Viwango vya kimataifa.

**62. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Afisi ilikadiria kukusanya na kuchangia katika Hazina ya Serikali jumla ya Tsh. 4,000,000.00 ambapo hadi kufikia Machi, 2009 fedha zilizokusanywa ni Tsh. 2,000,000.00 sawa na asilimia 50 ya makadirio. Makusanyo haya yalitarajiwa kufikia Tsh. 2,667,000.00 hadi mwezi Juni, 2009.

**63. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kutekeleza malengo ya kazi zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2009/2010, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinisha jumla ya Tsh. 1,007,000,000.00 kwa kazi za Kawaida na Tsh. 300,000,000 kwa kazi za maendeleo. Aidha Afisi katika mwaka 2009/2010 inakusudia kuchangia katika Hazina ya Serikali mapato ya Tsh. 4,000,000.00

#### **AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR**

**64. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mufti wa Zanzibar inajukumu kubwa la kutoa miongozo na kutatua migogoro mbali mbali ya kidini kwa wananchi wa Zanzibar. Hadi kufikia Machi, 2009 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

**Kuimarisha elimu ya dini katika jamii ya Kiislamu ndani na nje ya nchi.**

**65. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mufti imeendelea kushughulikia migogoro mbali mbali na kupatiwa ufumbuzi. Migogoro 153 imepokelewa na karibu migogoro yote iliyowasilishwa imepatiwa ufumbuzi. Afisi

imeendelea kupokea maswali mbali mbali kutoka kwa Wananchi ndani na nje ya nchi ambapo maswali 288 yaliulizwa na waumini wa hapa Visiwani na 27 kutoka Tanzania Bara na yote yamejibiwa.

**66. Mheshimiwa Spika,** Afisi imeendelea kuelimisha jamii kwa kutumia hotuba za Ijumaa, ziara za Mufti wa Zanzibar katika Misikiti ya Unguja na Pemba na kwa njia ya semina na makongamano juu ya kuepuka migogoro. Katika kushirikiana na taasisi za nje, wageni mbali mbali waliitembelea Afisi wakiwemo Balozi wa Saudi Arabia, Mkurugenzi wa 'World Islamic Call Society' tawi la Dar Es Salaam, Katibu Mkuu wa 'Union Of Muslim Council' (UMC) kutoka Uganda, ujumbe wa waislam kutoka Uingereza, Shirika la USAIDS na kikundi cha Masheikh kutoka Yemen. Aidha Mufti wa Zanzibar amehudhuria mkutano wa kidini nchini Libya (**World Islamic People Leadership**) na kuonana na Rais Gadafi na viongozi mbali mbali.

**67. Mheshimiwa Spika,** Afisi ilifanya mikutano ya ushauri ya wajumbe wa Baraza la Maulamaa, kuendesha semina kwa maeneo mbali mbali mijini na vijijini, Mufti kutembelea Misikiti ya Ijumaa, kufanya kongamano maalum juu ya umuhimu wa kuvumiliana, na kuelimisha viongozi wa dini juu ya matokeo ya utafiti wa hali ya migogoro ya kidini hapa nchini.

#### **Kuimarisha mazingira mazuri ya kufanyia kazi**

**68. Mheshimiwa Spika,** nina furaha kuliarifu Baraza lako kuwa Afisi ya Mufti sasa imeshahamia katika jengo lake jipya lililopo kwenye makutano ya barabara ya Amani na Kiembesamaki na ile ya Mazizini (Mbuyu-mnene). Afisi ya Mufti ilifunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Al hajji Dk. Aman Abeid Karume mwezi Machi mwaka huu katika hafla iliyohudhuriwa pia na ujumbe wa Serikali ya Oman ukiongozwa na Mufti Mkuu wa Nchi hiyo Sheikh Ahmed Moh'd Al-khalily. Aidha Afisi imepata msaada wa samani kutoka shirika la 'World Islamic Call Society' kutoka Libya na Ubalozzi mdogo wa Oman uliopo hapa Zanzibar.

**69. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kuwaendeleza wafanyakazi, Afisi imeendelea kuwasomesha wafanyakazi wake watano katika kozi tofauti za muda mrefu. (**Angalia kiambatanisho 6a**).

**Kuendelea na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa taratibu za Kiislamu**

**70. Mheshimiwa Spika**, Afisi iliendelea kuwafunza Maimamu wa Misikiti ya Ijumaa mafunzo ya UKIMWI kwa muongozo wa Kiislamu, kuziwezesha kitaaluma kamati za UKIMWI za wilaya za Unguja na Pemba, kufanya mkutano wa kawaida wa Kamati ya Kiufundi ya UKIMWI (TAC), kuendesha mkutano wa mapitio ya mpango wa utekelezaji na ufuatiliaji juu ya mapambano ya UKIMWI, na pia Mkutano wa Wafanyakazi wake Unguja na Pemba. Pia Afisi imechapisha na kuvigawa vipeperushi na vitabu vya Muongozo wa Kiislamu katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

**71. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Afisi imejiwekea malengo yafuatayo:

- a. Kuimarisha uwezo wa afisi kiutendaji
- b. Kuendelea na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa taratibu za Kiislamu;

**72. Mheshimiwa Spika**, Ili Afisi ya Mufti iweze kutekeleza kazi na malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2009/2010 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh. 141,483,200.00 kwa kazi za kawaida.

**IDARA YA URATIBU UTAWALA BORA**

**73. Mheshimiwa Spika**, idara hii ina jukumu la kujenga na kusimamia utekelezaji wa misingi ya utawala bora, katika mwaka huu wa fedha 2008/2009 imeweza kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo :-

**Kukuza uelewa na utekelezaji wa Utawala Bora katika Taasisi za Kiserikali na Zisizo za Kiserikali**

**74. Mheshimiwa Spika**, Idara imeweza kuzindua Kamati ya Kitaifa ya Elimu ya Uraia yenye jumla ya wajumbe kumi na nne (14). Kati yao wajumbe sita (6) wanatoka Serikalini na wajumbe wanane (8) wanatoka katika taasisi zisizo za Kiserikali. Jukumu kubwa la kamati hiyo ni kutoa miongozo

ya kisera katika utoaji wa elimu ya uraia ili kuimarisha uelewa wa Wazanzibari juu ya misingi ya haki na wajibu wao katika maendeleo.

**75. Mheshimiwa Spika,** Sambamba na uanzishwaji wa kamati hiyo Idara inatayarisha Mkakati wa Elimu ya Uraia hapa Zanzibar. Lengo kuu la Mkakati huo ni kutoa maelekezo ya namna ya utoaji wa Elimu ya Uraia Zanzibar na kuweka utaratibu mzuri wa kuratibu suala hilo. Wataalamu wakitayarisha Mkakati huo wameshachaguliwa na tayari kazi inaendelea.

**76. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho Idara imeweza kuzindua rasmi Muongozo wa Haki za Binaadamu kwa mujibu wa sura ya tatu ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kazi hii imefanyika kwa msaada wa Shirika la Mpango la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Hivi sasa tayari hatua za kuusambaza zimeanza. Aidha hatua za kuutolea elimu kwa njia ya redio nazo zimefanyika.

#### **Kuendelea na kazi ya Uratibu Utawala Bora Zanzibar**

**77. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Idara imeweza kukamilisha utayarishaji wa sera ya jumuiya zisizo za Kiserikali na tayari sera hiyo imeshachapishwa. Aidha kazi za kuisambaza kwa wadau kwa utekelezaji inaendelea. Lengo la Wizara ni kuona sheria iliokuwepo inafanyiwa marekebisho ili iendane na sera.

**78. Mheshimiwa Spika,** katika hotuba ya Bajeti ya mwaka jana nilieleza juu ya kazi ya kupitia upya rasimu ya Sheria ya Kupambana na Rushwa. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa msaada mkubwa waliotoa ambao umefanikisha kazi hii. Vile vile napenda kutoa taarifa kuwa kazi ya kufanya mapitio hayo sasa imekamilika. Hatua inayofuata ni kuifikisha rasimu hiyo katika vikao vinavyohusika.

#### **TUME YA HAKI ZA BINAADAM NA UTAWALA BORA**

**79. Mheshimiwa Spika,** Idara imekuwa na mashirikiano mazuri ya kiutendaji na Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora ya Tanzania. Tume kwa upande wake katika kipindi cha Julai 2008 hadi Machi 2009, imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu uvunjwaji wa Haki za Binaadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala bora na kuyafanyia kazi.

Katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Machi, 2009 Tume ilipokea malalamiko 35 na ilikamilisha uchunguzi wa malalamiko 10, malalamiko hayo yanahusiana zaidi na masuala ya kijamii mfano madai ya mafao mbalimbali, bima, haki ya umiliki na ajira. Jumla ya malalamiko ambayo uchunguzi wake ulikuwa unaendelea kufanyika hadi kufikia Machi, 2009 ni 252.

**80. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho Tume imeweza kutoa elimu ya Haki za Binaadamu na misingi ya Utawala Bora kwa wanajumuiya wa vyuo mbali mbali ili kuongeza elimu ya Utawala Bora. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Chuo Kikuu cha Zanzibar kilichopo Tunguu, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Chukwani, Chuo cha Taaluma ya Sayansi za Afya Mweni, Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka na Chuo cha Ufundi Karume. Hatua hii ya kutoa elimu kwa wanajumuiya wa vyuo ni ya awali ambapo muongozo wa kutoa elimu kwa wananchi kiujumla unaandaliwa.

#### **Kuimarisha Idara ya Uratibu Utawala Bora Kitaaluma na Vitendea Kazi**

**81. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha kitaaluma wafanyakazi wake, Idara imepeleka wafanyakazi watatu katika masomo ya muda mrefu kwa kiwango cha Shahada ya Uzamili. Kati ya hao mmoja anasomea Shahada ya Uzamili ya Uongozi na wawili wanasomea shahada ya Uzamili ya sheria (**Angalia kiambatanisho 6a na 6b**)

**82. Mheshimiwa Spika,** Idara katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 imekusudia kutekeleza mambo yafuatayo:-

- a) Kuendeleza uelewa na utekelezaji wa Utawala Bora katika Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali; na
- b) Kuimarisha uwezo wa Idara kiutendaji.

**83. Mheshimiwa Spika,** ili Idara hii iweze kutekeleza vyema malengo iliyojipangia katika kipindi cha mwaka 2009/2010 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 116, 203,000.00 kwa kazi za kawaida na Tsh. 110,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

## **AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI**

**84. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inasimamia na kushughulikia masuala yote ya usajili chini ya sheria mbali mbali za vizazi na vifo, tirka za mali maiti kwa wasiokuwa waislam, usajili wa makampuni na majina ya biashara, usajili wa alama za biashara na vielelezo vya uvumbuzi pamoja na kusimamia shughuli zinazohusu mali za ubunifu, usajili wa nyaraka mbali mbali, usajili wa ndoa na talaka, usajili wa jumuiya zisizo za kiserekali na kutoa ushauri wa maelekezo ya sheria kwa wananchi juu ya shughuli za Afisi.

**85. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2009 vyeti 45,000 vimesambazwa katika wilaya zote za Unguja na Pemba, ambapo vizazi 30,799 vimesajiliwa kati ya hivyo 14,864 ni wanaume na 15,955 ni wanawake. Aidha vifo 1,363 vimesajiliwa. Kwa upande wa urithi kwa wasiokuwa waislamu, jumla ya 'estate duty' 11 na Tirka 7 zilishughulikiwa. Aidha katika kipindi hicho yamesajiliwa Makampuni 166, majina ya Biashara 230, jumuiya zisizo za Kiserikali 73, alama za Biashara 355, na alama za uvumbuzi 20. Idadi ya nyaraka zilizosajiliwa ni 1222 ambapo nyaraka za dhamana za Benki (A1) ni 30 nyaraka za mauziano na urithi (A2) ni 561, nyaraka za Wakfu, hiba , kiapo, kodi nk (A3) ni 617 na waraka wa kufuta dhamana za Benki ni 14. Kwa upande wa ndoa na talaka jumla ya mabuku 108 ya ndoa na mabuku 6 ya talaka yametolewa katika kipindi hicho ambayo yametumika katika wilaya tofauti za Unguja na Pemba **(Angalia kiambatisho namba 9a na 9b).**

**86. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2009 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

**Kuimarisha uwezo wa Afisi kiutendaji.**

**87. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usajili wa makampuni na majina ya Biashara, Afisi imepokea kompyuta mbili pamoja na mashine ya fotokopi kupitia mradi wa kuimarisha utawala Bora unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB). Pia Afisi imekamilisha kazi ya tathmini ya kuwapata wataalamu kwa ajili ya kurekebisha mfumo na taratibu zinazoongoza usajili na uendeshaji biashara. Mkataba wa kazi hiyo baina ya Kampuni ya 'Norway Registry Development' na Wizara tayari

umeshawekwa saina kwa ajili ya kuanza kazi. Aidha mradi wa **“Digitization of Paper Records”** nao matayarisho yake yapo katika hatua za mwisho.

**88. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Afisi imefanya matengenezo makubwa katika chumba chake cha kuhifadhi kumbukumbu (strong room) kwa ajili ya kukiimarisha na kuwezesha kumbukumbu kuwa katika hali ya kuridhisha. Afisi pia inaendeleza ujenzi wa jengo lake la Afisi ya Pemba ambao ulikuwa umesita na hivi sasa hatua inayoendelea ni kuliezeka. Juhudi za kupata jengo jipya kukidhi mahitaji ya Afisi zinaendelea kuchukuliwa.

**Kuendelea kuzifanyia marekebisho Sheria mbali mbali zinazosimamiwa na Afisi.**

**89. Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha kwamba sheria zinazosimamiwa zinakidhi mahitaji kwa wakati tulionao, mchakato wa kutayarisha Sheria ya kuanzishwa kwa Afisi ya Mraji Mkuu wa Serikali na Sheria ya Makampuni na majina ya Biashara unaendelea.

**Kuimarisha utumiaji wa teknolojia katika mifumo ya usajili.**

**90. Mheshimiwa Spika,** Afisi imewapatia mafunzo wafanyakazi wanaohusika na usajili wa vizazi na vifo kwa Wilaya zote Unguja na Pemba katika utumiaji wa mfumo mpya wa usajili. Zoezi hili lilikuwa muhimu ili kuhakikisha vifaa vilivyopo vinatunzwa na vinatumika kwa uangalifu na usajili unaimarishwa.

**Kutoa elimu ya shughuli za Afisi ya Mraji Mkuu wa Serikali.**

**91. Mheshimiwa Spika,** Afisi imewapatia semina mashekhe wanaosajili ndoa na talaka katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba kwa lengo la kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili eneo hilo zikiwemo athari za kutumia mabuku ya ndoa na talaka ambayo hayatolewi na Afisi, kutorudisha malipo yatokanayo na ada zinazotowwa katika usajili huo pamoja na vitabu vya ndoa na talaka kwa ajili ya kumbukumbu na kuthibitisha vyeti ambavyo ni vivuli vitokanavyo na vyeti halisi (certified copy).

**92. Mheshimiwa Spika**, Makadirio ya mapato kwa mwaka 2008/2009 ni Tsh. 247,728,000.00, hadi kufikia Machi, fedha zilizokusanywa ni Tsh. 170,388,608.00 sawa na asilimia 69 ya makisio ya mwaka 2008/2009. Afisi pia ilikadiri kukusanya jumla ya Tsh. 227,184,810.67 hadi kufikia mwezi Juni, 2009 sawa na asilimia 91.707 (**Angalia kiambatisho namba 3**)

**93. Mheshimiwa Spika**, Afisi inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

- a. Kuimarisha uwezo wa Afisi kiutendaji.
- b. Kuendeleza mradi wa usajili wa vizazi na vifo.
- c. Kuendelea kuzipitia sheria zinazoongoza kazi za usajili.
- d. Kuikamilisha sheria ya uanzishwaji wa Sheria ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali.

**94. Mheshimiwa Spika**, ili Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali iweze kutekeleza majukumu yake niliyoyataja hapo juu kwa mwaka 2009/2010, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Tsh. 286,339,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Tsh. 60,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inakusudia kuchangia katika Hazina ya Serikali mapato ya Tsh. 285,400,000.00 kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya mapato.

#### **AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI**

**95. Mheshimiwa Spika**; Afisi ya Msajili wa Hakimiliki ina majukumu ya kulinda na kusimamia matumizi halali ya kazi za sanaa na kukusanya na kugawa mirabaha kutoka kwa watumiaji mbali mbali wa kazi hizo. Hadi kufikia Machi, 2009 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

#### **Kuimarisha utendaji wa Afisi**

**96. Mheshimiwa Spika**, Afisi ya Hakimiliki imempeleka mafunzoni mfanyakazi mmoja katika ngazi ya Shahada ya Uzamili. Afisi pia imewapeleka wafanyakazi wanne kwenye Chama cha Hakimiliki nchini Malawi kwa mafunzo ya muda mfupi juu ya usimamizi wa hakimiliki na hakishiriki (**Angalia kiambatanisho 6a na 6b**). Aidha afisi imeajiri wafanyakazi watatu (3), wawili kwa Unguja na mmoja kwa Pemba.

**97. Mheshimiwa Spika,** Afisi imeendelea kuipitia mikataba mbalimbali ya wasanii na kutayarisha mikataba kwa wasanii ambao wameshasajili kazi zao na wasiosajili. Mikataba minne (4) imepitiwa na kuwarejeshea wahusika kabla ya wahusika hao kuingia kwenye mikataba hiyo. Aidha Afisi imepokea na kufanyia kazi malalamiko kumi na nne (14) yanayohusu utumikaji wa kazi za sanaa pasipo na ridhaa za wasanii wenyewe. Kwa upande mwingine afisi imesajili kazi mbalimbali za sanaa ambazo muziki ni 80, miswada ya mashairi 4, rikodi 5 za kasida na moja ya filamu na miswada ya filamu 5. Afisi imeendelea na kazi ya kuelimisha jamii juu ya dhana na Sheria ya Hakimiliki kupitia programu za televisheni na kutoa vipeperushi. Jumla ya vipindi kumi na mbili vilitayarishwa na kurushwa hewani.

#### **Kuimarisha mfumo wa usajili wa kazi za ubunifu na kuanza utoaji wa leseni**

**98. Mheshimiwa Spika,** kwa kuanzia Afisi imekuwa ikitumia mfumo wa elektroniki wa usajili uliyotayarishwa na Afisi kuanzia mwaka 2007. Hata hivyo katika kuleta ufanisi wa usajili kwa ulinzi wa kitaifa na kimataifa wa kazi za sanaa, Afisi imeomba mfumo wa usajili unaosimamiwa na WIPO (WIPOCOS), ambao unaotumiwa na nchi zote wanachama wa mkataba wa 'Berne'. Mfumo huo utarahisisha kuzitambua kazi za nje ambazo zinahitaji kulindwa nchini na kutoa fursa ya usimamizi mzuri wa kazi za wasanii wetu nchi za nje. Mafunzo ya usimamizi wa mfumo huo kwa watendaji wa Afisi yanatarajiwa kutolewa na wataalamu wa WIPO kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha.

**99. Mheshimiwa Spika,** Afisi imezindua rasmi utoaji wa leseni za matumizi halali ya kazi za sanaa kwa watumiaji wote wa kibiashara. Leseni hizo kwa kuanzia zitatolewa kwa Vyombo vya habari vya umma na vya binafsi vikiwemo Zanzibar Cable, kampuni ya simu ya Zantel, Tamasha la Filamu Zanzibar na tamasha la Busara pamoja kumbi za burudani. Leseni kwa wenye mahoteli zitatolewa kwa utaratibu maalum ulioandaliwa na "Copyright Task force". Kazi hii inatarajiwa kukamilika kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha.

## **Kukuza uelewa wa jamii juu ya dhana na Sheria ya Hakimiliki**

**100. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kwamba elimu juu ya dhana na sheria ya Hakimiliki inafika kwa walengwa, Afisi imefanya warsha katika Mkoa wa Kaskazini Unguja mwezi Julai, 2008. Pia imeendesha warsha hizo katika mkoa wa Kaskazini na kusini Pemba na kufanya idadi ya mikoa iliyopatiwa taaluma hiyo kufikia minne na kubaki mkoa mmoja wa Kusini Unguja. Aidha Afisi pia imefanya mikutano ya elimu hiyo kwa masheha wa shehia 140 za mikoa miwili ya Unguja.

### **Kuendesha utafiti wa kuelewa kiwango cha ubunifu Zanzibar na mchango wake kwa uchumi wa taifa**

**101. Mheshimiwa Spika**, kwa kubaini haja ya kuelewa kiwango cha ubunifu Zanzibar na mchango wake kwa uchumi wa Taifa, Afisi kwa kushirikiana na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inaendesha zoezi la ukusanyaji wa taarifa za kuelewa kiwango cha ubunifu Zanzibar kwa mikoa ya Kaskazini na Mjini Magharibi Unguja. Taarifa zilizokusanywa ziko katika hatua ya uchambuzi ambapo zoezi hili litaendelea kwa mikoa mitatu iliyobakia na hatimae kuandaa taarifa hizo kwa matumizi ya Serikali.

**102. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka ujao wa fedha 2009/2010 Afisi imejipangia malengo yafuatayo;

- a) Kuimarisha uwezo wa Afisi kiutendaji na kuandaa mpango wa kimkakati
- b) Kutoa na kusimamia utekelezaji wa utoaji wa leseni
- c) Kuendeleza utafiti wa kuelewa kiwango cha ubunifu Zanzibar kwa mikoa mitatu na mchango wake kwa uchumi wa taifa.

**103. Mheshimiwa Spika**, ili Afisi iweze kumudu na kutekeleza vyema mipango na majukumu yake hayo katika kipindi cha 2009/2010 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishhe ruzuku ya Tsh. 120,000,000.00.

## **KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA**

**104. Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina jukumu la kusimamia Nyakfu na Amana mbali mbali pamoja na kushughulikia masuala ya Waislamu yakiwemo Miradhi, Hija, Sadaka na Zakka na kusimamia Sala na Mabaraza ya Iddi ya Kitaifa. Hadi kufikia Machi, 2009 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

### **Kuongeza uwezo na uelewa wa Sheria ya Kamisheni kwa wadau wake**

**105. Mheshimiwa Spika,** Kamisheni imekuwa ikiendelea na ujazaji wa mikataba mipya ya upangaji wa nyumba zilizo chini yake. Hadi kufikia Machi 2009 wapangaji waliojaza mikataba yao ni 275 sawa na asilimia 45 na ambao hawajajaza mikataba yao ni 336 sawa na asilimia 55 Aidha, Kamisheni inakusudia kuwafikisha mbele ya vyombo vya Sheria wapangaji wote ambao watakaoshindwa kujaza mikataba mipya hadi ifikapo mwezi Agosti 2009.

**106. Mheshimiwa Spika,** kazi ya usimamizi wa kesi katika Mahakama mbali mbali inaendelea ambapo kesi (5) zimetolewa maamuzi na kesi (20) zinaendelea kwa mchanganuo ufuatao: Mahakama Kuu (kesi 11); ambapo kesi (7) za Mirathi, kesi (3) za Misikiti, kesi (1) ya Wakfu. Mahakama ya Naibu Kadhi Mkuu kesi (5) za mirathi. Mahakama ya Kadhi wa Wilaya kesi (2) za mirathi; Mahakama ya Ardhi kesi (1) inayohusiana na umiliki wa nyumba; Bodi ya kudhibiti kodi za nyumba kesi (1) juu ya uhalali wa upangaji wa nyumba ya Wakfu. Aidha, Kamisheni imefanya Semina mbili za kuitangaza Sheria ya Wakfu Nam. 2 ya 2007 kwa Makamanda wa Jeshi la Polisi Unguja na Pemba. Nakala za Sheria mpya ya Kamisheni ziligaiwa kwa makamanda hao Unguja na Pemba.

### **Kuimarisha Utendaji wa Kamisheni**

**107. Mheshimiwa Spika,** Katika hali ya kunyanyua viwango vya elimu wafanyakazi watatu (3) wamepelekwa kwenye mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya stahhada (**Angalia kiambatanisho 6a na 6b**).

**108. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya Tirka 389 zenye thamani ya Tsh. 1,172,552,930.45 zimefunguliwa ambapo kati yake tirka 315 zimefungwa na ushuru wake ni Tsh. 54,713,236.70. Aidha, mizozo 31 kuhusu mirathi imepokelewa, kati ya hayo 19 imesuluhishwa na kumi na mbili (12) imepelekwa Mahakamani, na saba (7) imeshatolewa uamuzi.

**109. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Hijja Jumla ya Mahujaji 1311 walikwenda kufanya Ibada Tukufu ya Hijja kwa mwaka 2008 sawa na 1429H (**Kiambatanisho Nam 10a**). Kamisheni pia imesimamia na kuendesha kwa ufanisi sala na Mabaraza ya Idd –El Fitri na Idd – El- Hajj kitaifa.

**110. Mheshimiwa Spika,** katika hali ya kujenga na kuendeleza mahusiano mema na jamii, Kamisheni imeziomba msamaha wa ushuru wa Forodha na kodi ya mauzo Jumuiya 5 (**Kiambatanisho Nam 10b**) Kamisheni imetoa barua ishirini na nne (24) za kuwaomba wananchi msaada wa matibabu; barua kumi na nane (18) za misaada ya ujenzi wa Misikiti na Vyuvo vya Qur-ani kwa maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba; na imewapatia Watoto Mayatima barua ishirini na tatu (23) za kuwaomba msaada wa kimaisha. Kamisheni ilipokea sadaka ya tende boksi 500 (kilogram 6,000) ambapo boksi 201 zilipelekwa kisiwani Pemba na boksi 299 ziligaiwa hapa Unguja. Kadhalika, Kamisheni imepokea sadaka ya nyama ya kondoo boksi 2655 na iligaiwa bosi 1014 kwa Unguja na 776 kwa Pemba.

**111. Mheshimiwa Spika,** Kamisheni imekuwa ikiendelea na ujenzi wa nyumba ya Wakfu huko Mbweni ambayo tayari imeshaezekwa na hatua inayofuata sasa ni kazi za umaliziaji. Aidha, Kamisheni imeendelea kufuatilia upatikanaji wa viwanja ishirini na tano huko Idara ya Ardhi na Usajili kwa ajili ya kujenga nyumba na kuwakodisha wananchi ili kupunguza tatizo la makaazi na kuiongezea kipato Kamisheni.

#### **Kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizo ya virusi vya UKIMWI**

**112. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha 2008/2009, Kamisheni ilifanya semina mbili ili kuwaelimisha wafanyakazi wake. Aidha, ilitoa elimu ya kujjepusha na maambukizo mapya ya UKIMWI na athari za unyanyapaa

wa wagonjwa wa UKIMWI kwa walimu na wanafunzi wa madrasa (za Qur-an) za Unguja na Pemba.

**113. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka ujao wa fedha wa 2009/2010, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imejiwekea malengo yafuatayo:-

- a. Kuendelea kuongeza uwezo na uelewa wa sheria ya Kamisheni kwa wadau.
- b. Kuendelea kuimarisha utendaji wa Kamisheni; na
- c. Kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizo ya virusi vya UKIMWI.

**114. Mheshimiwa Spika,** ili Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iweze kumudu na kutekeleza vyema mipango na majukumu yake katika kipindi cha 2009/2010, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinisha ruzuku ya Tsh. 274,000,000.00.

#### **AFISI KUU PEMBA**

**115. Mheshimiwa Spika,** Afisi Kuu ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba na kuwa kiungo kati ya taasisi za ndani na zile za nje ya Wizara. Hadi kufikia Machi, 2009 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:

#### **Kuimarisha uwezo wa Afisi katika kuratibu shughuli za kazi za Wizara Pemba**

**116. Mheshimiwa Spika,** kufuatia kuteuliwa kwa Naibu Mufti Pemba, wananchi wengi wameweza kuelewa na kuitumia vizuri Afisi ya Mufti, jumla ya masuala 69 yamepokelewa na tayari yote yametolewa fatwa, pia migogoro 22 na mizozo ya ndoa 38 imepokelewa na yote imetatuliwa. Aidha napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba sasa Naibu Mufti amepatiwa usafiri wa uhakika na tatizo la usafiri limemaliza.

**117. Mheshimiwa Spika,** katika kuratibu jumuiya zisizo za kiserikali, Afisi imekuwa ikizihamasisha Jumuiya kutumia vyema fedha wanazozipata katika miradi mbali mbali, ili kuleta maendeleo kwa jamii, Jumuiya 8 zimesaidiwa katika kuandaa katiba na kupatiwa usajili. Aidha malalamiko mawili ya jumuiya za kiraia yamepokelewa na yote yamepatiwa ufumbuzi.

**118. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Afisi imeratibu shughuli za Wizara kwa ufanisi kwa kuratibu mikutano ya Wakuu wa taasisi, kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo, Ununuzi wa kompyuta, jenereta na vitendea kazi mbali mbali. Aidha Afisi imepatiwa gari moja mpya kwa ajili ya kupunguza tatizo la usafiri kwa watendaji wake.

**Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma.**

**119. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2008/2009 jumla ya wafanyakazi wawili wanaume wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya stahhada na wafanyakazi 6 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Aidha mfanyakazi mmoja anaendelea na mafunzo ya vitendo (Internship) ya mwaka mmoja katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (**Angalia kiambatanisho 6a na 6b**).

**Kuendelea na mpango wa kutoa taaluma ya elimu ya UKIMWI**

**120. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2008/2009 jumla ya semina tatu zimefanywa katika kuhamasisha Wafanyakazi kujikinga na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI, mafunzo hayo yalikusishwa wafanyakazi na familia zao pamoja na kamati ya UKIMWI ya Wizara. Uhamasishaji huo umeleta muamko kwa wafanyakazi katika kujikinga na UKIMWI na kuondoa unyanyapaa.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Afisi Kuu Pemba, imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a. Kuendelea kusimamia na kuratibu utendaji wa taasisi za Wizara
- b. Kuendelea na kutoa taaluma ya Ugonjwa wa UKIMWI

**122. Mheshimiwa Spika,** Ili Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza malengo iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2009/2010 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilling 203,353,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

## CHANGAMOTO

**123. Mheshimiwa Spika,** pamoja na ufanisi katika kutekeleza malengo tuliyojiwekea kwa mwaka 2008/2009, Wizara ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:

- i. Kutokupatikana fedha za wafadhili kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama.
- ii. Ufinyu wa ruzuku inayotolewa kwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kiasi cha kushindwa kukidhi mahitaji yake muhimu.
- iii. Uhaba wa vitendea kazi hasa kompyuta kwa Afisi ya Mdhibiti ili kuwezesha kukamilisha kazi kwa wakati.
- iv. Ufinyu wa bajeti kwa Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali.
- v. Uhaba wa Vyombo vya Usafiri kwa watendaji wa Taasisi za Wizara

## SHUKURANI

**124. Mheshimiwa Spika,** sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuiwasilisha Hotuba hii mbele ya Baraza lako Tukufu. Aidha haitokuwa jambo la busara kama sitatoa shukurani zangu za dhati kwa wale wote waliotoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara pamoja na Taasisi zake zote. Shukurani maalum nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako Tukufu. Sambamba na hilo natoa shukurani kwa watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa taasisi za Wizara yangu kwa hatua nzuri za kiutendaji. Vilevile kwa niaba ya watendaji wa Wizara yangu napenda kutoa shukurani kwa wajumbe wa Baraza hili kwa michango yao mizuri na yenye manufaa kwa Wizara na Taifa kwa ujumla.

**125. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imekuwa ikifanya kazi zake kwa mashirikiano na wafadhili na wahisani mbalimbali na kwa heshima na taadhima naomba ruhusa yako kuwashukuru wale wote wanaotusaidia wakiwemo UNDP, ADB, WIPO, GLOBAL FUND, WORLD BANK, Africa Muslims Agency, Al - Youseif Charitable Society, Serikali ya Oman, Serikali ya Saud Arabia, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania, Swedish National Audit Office (SNAA),

Islamic Development Bank, Tume ya UKIMWI ya Zanzibar (ZAC) na Vikundi mbalimbali vilivyosafirisha Mahujaji.

## **HITIMISHO**

**126. Mheshimiwa Spika, kwa** kumalizia naomba wajumbe wa Baraza lako Tukufu waidhinishhe matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 ya jumla ya Tsh. 5,128,017,200 kwa kazi za kawaida na Tsh. 1,460,000,000 kwa kazi za maendeleo ili iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia. Aidha naliomba Baraza lako likubali mchango wa Tsh. 331,400,000.00 ikiwa ni mapato yatakusanywa na Wizara hii ambayo yataingizwa katika Hazina ya Serikali.

**127. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**RAMADHAN ABDALLA SHAABANI**

**WAZIRI WA NCHI (AR)**

**KATIBA NA UTAWALA BORA**

**ZANZIBAR.**

**KIAMBATISHO 1: FEDHA ZILIZOINGIZWA KWA MATUMIZI YA KAWAIDA**

FUNGU	IDARA	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2008/2009			JUMLA FEDHA ZILIZOINGIZWA JUL - MAC 2008/2009	WASTANI WA JUMLA (%)	MCHANGANUO WA FEDHA ZILIZOINGIZWA			
		JUMLA	MSHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO			MISHAHARA NA MAPOSHO	(%)	MATUMIZI MENGINEYO	(%)
11	Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	900,000,000	443,073,000	456,927,000	635,909,234	71%	296,582,234	67%	339,327,000	74%
14	Mahkama	1,134,402,000	798,430,111	335,971,889	816,951,094	72%	572,234,094	72%	244,717,000	73%
15	Afisi ya Mwanasheria Mkuu	550,450,000	167,190,000	383,260,000	325,699,024	59%	129,699,032	78%	195,999,992	51%
35	Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	508,000,000	196,210,817	311,789,183	385,169,835	76%	161,287,060	82%	223,882,775	72%
33/04	Mipango na Sera	415,749,000	178,443,000	237,306,000	260,804,238	63%	137,401,110	77%	123,403,128	52%
33/05	Afisi ya Mufti wa Zanzibar	136,774,000	81,098,000	55,676,000	88,547,452	65%	59,318,759	73%	29,228,693	52%
33/07	Idara ya Uratibu Utawala Bora	117,790,000	47,003,000	70,787,000	75,400,684	64%	32,452,798	69%	42,947,886	61%
33/09	Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili	11,672,000	11,672,000	0	8,240,898	71%	8,240,898	71%	0	0
33/11	Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali	270,580,000	138,204,000	132,376,000	164,347,368	61%	97,734,635	71%	66,612,733	50%
33/03	Afisi Kuu Pemba	204,435,000	106,832,000	97,603,000	124,900,141	61%	85,976,641	80%	38,923,500	40%
Ruzuku	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	214,000,000	155,934,786	58,065,214	120,711,458	56%	102,611,458	66%	18,100,000	31%
Ruzuku	Afisi ya Msimamizi wa Hakimiliki	120,000,000	18,615,252	101,384,748	85,934,559	72%	14,955,130	80%	70,979,429	70%
	<b>JUMLA</b>	<b>4,583,852,000</b>	<b>2,342,705,966</b>	<b>2,241,146,034</b>	<b>3,092,615,985</b>	<b>67%</b>	<b>1,698,493,849</b>	<b>73%</b>	<b>1,394,122,136</b>	<b>62%</b>

## Kiambatisho 2: Fedha za Miradi

JINA LA MRADI	MAKISIO 2008/2009			MATUMIZI HALISI (JULAI 2008 – MACHI 2009)					MUHSANI
	SMZ	MUHSANI	JUMLA	SMZ	%	MUHSANI	%	JUMLA	
Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	120,000,000	600,000,000	720,000,000	120,000,000	100	250,000,000	42	370,000,000	Sweden/ADB
Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora	100,000,000	65,000,000	165,000,000	95,000,000	95	27,639,000	43	122,639,000	UNDP
Mradi wa Kuimarisha Mahakama	83,000,000	117,000,000	200,000,000	65,000,000	78		0	65,000,000	ADB
Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	200,000,000	235,691,346	435,691,346	75,000,000	38	235,691,346	100	310,691,346	UNDP
Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka	300,000,000	143,171,000	443,171,000	230,000,000	77	60,346,675	42	290,346,675	ADB
<b>Jumla Kuu</b>	<b>803,000,000</b>	<b>1,160,862,346</b>	<b>1,963,862,346</b>	<b>585,000,000</b>	<b>73</b>	<b>573,677,021</b>	<b>49</b>	<b>1,158,677,021</b>	<b>59%</b>

**Kiambatisho 3: Makusanyo ya Mapato (2008/2009) na Makadirio ya 2009/2010**

<b>KIFUNGU</b>	<b>IDARA/TAASISI</b>	<b>MAKADIRIO</b>	<b>MAKUSANYO HALISI</b>	<b>ASILIMIA</b>	<b>MAKADIRIO 2009/2010</b>
33/11	<b>MRAJIS MKUU WA SERIKALI</b>	247,728,000.00	170,388,608.00	69	285,400,000.00
11	<b>AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU</b>	4,000,000.00	2,000,000.00	50	4,000,000.00
14	<b>MAHAKAMA</b>	41,200,000.00	25,937,814	63	42,000,000.00
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>292,928,000.00</b>	<b>198,326,422.00</b>	<b>68</b>	<b>331,400,000.00</b>

**KIMBATISHO 4: MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO 2009/2010**

FUNGU	IDARA	KAZI ZA KAWAIDA					KAZI ZA MAENDELEO			
		JUMLA	MSHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	MCHANGO WA SERIKALI	WAHISANI	JUMLA FEDHA ZA MAENDELEO	JUMLA KUU
11	Afisi ya Mdhifiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	1,007,000,000	469,301,000	537,699,000	1,007,000,000	-	300,000,000	600,000,000	900,000,000	1,907,000,000
14	Mahakama Kuu	1,298,000,000	914,506,000	383,494,000	1,298,000,000	-	550,000,000		550,000,000	1,848,000,000
15	Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	546,000,000	146,731,000	399,269,000	546,000,000	-	140,000,000		140,000,000	686,000,000
35	Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	653,000,000	272,000,000	381,000,000	653,000,000	-	300,000,000	490,000,000	790,000,000	1,443,000,000
33/03	Afisi Kuu Pemba	203,353,000	105,750,000	97,603,000		203,353,000			0	203,353,000
33/04	Idara ya Mipango na Sera	470,967,000	204,449,000	266,518,000	470,967,000	-			0	470,967,000
33/05	Afisi ya Muffi wa Zanzibar	141,483,200.00	75,592,000	65,891,200.00	136,466,000	-			0	141,483,200
33/07	Idara ya Uratibu Utawala Bora	116,203,000	45,416,000	70,787,000	116,203,000		110,000,000		110,000,000	226,203,000
33/09	Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili	11,672,000	11,672,000	0	11,672,000	-			0	11,672,000
33/11	Afisi ya Mraji Mkuu wa Serikali	286,339,000	130,923,000	155,416,000	232,553,000	53,786,000	60,000,000	1,116,393,876	1,176,393,876	1,462,732,876
Ruzuku	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	274,000,000	0	274,000,000	210,000,000	64,000,000			0	274,000,000
Ruzuku	Afisi ya Msimamizi wa Hakimiliki	120,000,000	0	120,000,000	120,000,000				0	120,000,000
	<b>JUMLA VOTE 33</b>	<b>1,624,017,200</b>	<b>573,802,000</b>	<b>1,050,215,200</b>	<b>1,297,861,000</b>	<b>321,139,000</b>	<b>170,000,000</b>	<b>1,116,393,876</b>	<b>1,286,393,876</b>	<b>2,910,411,076</b>
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>5,128,017,200</b>	<b>2,376,340,000</b>	<b>2,751,677,200</b>	<b>4,801,861,000</b>	<b>321,139,000</b>	<b>1,460,000,000</b>	<b>2,206,393,876</b>	<b>3,666,393,876</b>	<b>8,794,411,076</b>

**Angalizo:** Kiwango cha kubadilisha USD ni Tshs. 1326 (Viwango vya Benki Kuu 28 Mei 2009)

DPP \$ 360,000

Mraji Mkuu \$ 841,926

**KIAMBATISHO 5: MIRADI YA MAENDELEO 2009 - 2010**

<b>Namba ya Mradi</b>	<b>Jina la Mradi</b>	<b>Mchango wa Serikali</b>	<b>Mchango wa Wahisani</b>	<b>Mhisani</b>	<b>Jumla Kuu</b>
72210	Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mdhidhi na Mkagiuzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	300,000,000.00	600,000,000.00	World Bank, NORAD	900,000,000.00
72200	Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora	110,000,000.00	-	UNDP/GP.5	110,000,000.00
	Mradi wa Kurekebisha Mazingira ya Biashara	60,000,000.00	1,116,393,876.00	World Bank	1,176,393,876.00
72187	Mradi wa Kuimarisha Mahakama	550,000,000.00			550,000,000.00
72185	Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	140,000,000.00		UNDP	140,000,000.00
72212	Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	300,000,000.00	490,000,000.00	ADB	790,000,000.00
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>1,460,000,000.00</b>	<b>2,206,393,876.00</b>		<b>3,666,393,876.00</b>

**KIAMBATISHO NAMBA 6a: IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO YA MUDA MREFU 2008/2009**

IDARA/TAASISI	SHAHADA YA UZAMILI		STASHAHADA YA UZAMILI		SHAHADA YA KWANZA		STASHAHADA YA JUU		STASHAHADA		CHETI		JUMLA
	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	
Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	3	3				3			5	5			19
Mahakama						2	1			1	4	1	8
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	2	2								1			5
Afisi Kuu Pemba										2			2
Idara ya Mipango na Sera				1	1				3	1	1		7
Afisi ya Mufti wa Zanzibar				1		1			1	2			5
Idara ya Uratibu Utawala Bora		3				2							5
Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kisimamia Maadili ya Viongozi						1			1				2
Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali		2			1					1			4
Afisi ya Hakimiliki	1												1
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	3	3			1					1			8
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana							1		1	1			3
<b>JUMLA</b>	<b>9</b>	<b>13</b>	<b>0</b>	<b>2</b>	<b>3</b>	<b>9</b>	<b>2</b>	<b>0</b>	<b>11</b>	<b>14</b>	<b>5</b>	<b>1</b>	<b>69</b>

**KIAMBATISHO NAMBA 6b: IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO YA MUDA MFUPI 2008/2009**

NA	IDARA/TAASISI	W/KE	W/ME	JUMLA
1	Afisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	16	30	<b>46</b>
2	Mahakama	2	0	<b>2</b>
3	Afisi ya Mwanasheria Mkuu	4	4	<b>8</b>
4	Afisi Kuu Pemba	2	2	<b>4</b>
5	Idara ya Mipango na Sera	1	0	1
6	Afisi ya Mufiti wa Zanzibar	0	0	<b>0</b>
7	Idara ya Uratibu Utawala Bora	0	3	<b>3</b>
8	Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili	0	0	<b>0</b>
9	Afisi ya Mrajiis Mkuu wa Serikali	0	0	<b>0</b>
10	Afisi ya Haki Miliki	2	2	<b>4</b>
11	Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	3	8	<b>11</b>
12	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	0	0	<b>0</b>
	<b>JUMLA</b>	<b>30</b>	<b>49</b>	<b>79</b>

**KIAMBATISHO NAMBA 7a:UFUNGUAJI WA KESI KATIKA MAHAKAMA MBALIMBALI JULAI 2008 HADI MACHI 2009**

Mahakama	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
	Madai			Jinai		Madai		Jinai	
	Jumla	Zilizofun guliwa	Zilizotolew a Uamuzi	Zilizofun guliwa	Zilizotolew a Uamuzi	Zilizofung uliwa	Zilizotole wa Uamuzi	Zilizofung uliwa	Zilizotole wa Uamuzi
Mahakama ya Rufaa	9	0	0	0	0	5	0	4	0
M/Kuu Vuga	219	35	5	120	10	33	2	31	7
M/Kuu Pemba	32	3	1	23	5	3	0	3	0
Mahakama ya Kazi	12	12	2	0	0	0	0	0	0
Kadhi Mkuu	31	0	0	0	0	31	14	0	0
Mahakama Kadhi Rufaa Pemba	5	0	0	0	0	5	2	0	0
Mahakama Mkoa Vuga	253	23	7	157	17	50	16	23	9
Mahakama Mkoa Mfenesini	73	5	1	60	40	3	1	5	2
Mahakama Mkoa Mwera	116	5	0	105	23	2	0	4	3
Mahakama Mkoa Wete	52	1	0	48	19	3	0	0	0
Mahakama Mkoa Chake	57	1	0	46	21	3	1	7	3
Mahakama Wilaya Mw/kwe	360	34	10	319	124	7	2	0	0

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
	Madai			Jinai		Madai		Jinai	
<b>Mahakama</b>	<b>Jumla</b>	<b>Zilizofun guliwa</b>	<b>Zilizotolew a Uamuzi</b>	<b>Zilizofun guliwa</b>	<b>Zilizotolew a Uamuzi</b>	<b>Zilizofung uliwa</b>	<b>Zilizotole wa Uamuzi</b>	<b>Zilizofung uliwa</b>	<b>Zilizotole wa Uamuzi</b>
Mahakama Wilaya Mwera	78	3	1	70	75	5	1	0	0
Mahakama Wilaya Mkokotoni	164	1	0	162	102	1	0	0	0
Mahakama Wilaya Mfenesini	182	23	9	154	100	3	1	2	1
Mahakama Wilaya Makunduchi	95	0	0	93	69	1	0	1	1
Mahakama Wilaya Mkoani	47	0	0	47	22	0	0	0	0
Mahakama Wilaya Chake	64	2	0	59	17	2	0	1	0
Mahakama Wilaya Wete	101	1	0	98	52	0	0	2	0
Mahakama Wilaya Konde	69	1	0	68	51	0	0	0	0
Mahakama ya Watoto Yuga	13	0	0	13	1	0	0	0	0
Mahakama ya Watoto Mwera	18	0	0	18	1	0	0	0	0
Mahakama ya Watoto Mfenesini	7	0	0	7	5	0	0	0	0
Mahakama ya Watoto Wete	2	0	0	2	0	0	0	0	0
<b>Jumla</b>	<b>2059</b>	<b>150</b>	<b>36</b>	<b>1669</b>	<b>754</b>	<b>157</b>	<b>40</b>	<b>83</b>	<b>26</b>

KIAMBATISHO 7b: UFUNGUAJI WA KESI KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO						KIAMBATISHO 7c: UFUNGUAJI WA KESI KATIKA MAHAKAMA ZA KADHI WA WILAYA		
KESI ZILIZOFUNGULIWA								
Mahakama ya Mwanzo	Madai		Jinai		Mahakama za Kadhi Wilaya	Kesi zilizofunguliwa Madai		
	Jumla	Zilizo	Zilizo	Zilizo		Zilizo	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa uamuzi
		funguliwa	tolewa	funguliwa		tolewa		
		uamuzi		uamuzi				
Mwanakwerekwe	181	38	14	143	109	Mjini	625	257
Mwera	278	18	5	260	150	Mwera	5	4
Makunduchi	65	9	4	56	33	Mfenesini	22	17
Chwaka	75	6	4	69	53	Mkokotoni	40	30
Mfenesini	239	6	3	233	209	Makunduchi	14	9
Mkokotoni	124	7	2	117	101	Chake chake	5	2
Mkoani	55	11	8	44	35	Mkoani	49	34
Kengeja	13	3	3	10	10	Kengeja	5	4
Chake chake	39	3	2	36	7	Chwaka	73	49
Wete	100	6	2	94	52	Wete	98	52
Konde	39	8	5	31	23	Konde	33	8
<b>Jumla</b>	<b>1208</b>	<b>115</b>	<b>52</b>	<b>1093</b>	<b>782</b>	<b>Jumla</b>	<b>969</b>	<b>466</b>

**KIAMBATISHO NAMBA 8: KESI ZILIZOFUNGULIWA NA KUSIMAMIWA NA  
AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA JULAI 2008 HADI  
MACHI 2009**

<b>MAHAKAMA</b>	<b>IDADI YA KESI</b>
MAHAKAMA YA RUFAA TANZANIA	4
MAHAKAMA KUU YA VUGA	92
MAHAKAMA KUU PEMBA	19
MAHAKAMA YA MKOA VUGA	94
MAHAKAMA YA MKOA MWERA	99
MAHAKAMA YA MKOA MFENESINI	73
MAHAKAMA YA MKOA WETE	23
MAHAKAMA YA MKOA CHAKE CHAKE	38
MAHAKAMA WILAYA MWANAKWEREKWE	336
<b>JUMLA</b>	<b>778</b>

**KIAMBATISHO NAMBA 9a: VIZAZI NA VIFO VILIVYOSAJILIWA KIWILAYA**

Wilaya	Vizazi			Vifo		
	wanawake	wanaume	Jumla	wanawake	wanaume	Jumla
Mjini	6,700	6,048	12,748	248	301	549
Magharibi	1,653	1,322	2,975	50	35	85
Kaskazini A	1,012	880	1,892	42	55	97
Kaskazini B	543	550	1,093	25	19	44
Kusini	290	240	530	18	21	39
Kati,	278	243	521	12	18	30
<b>Jumla Unguja</b>	<b>10,476</b>	<b>9,283</b>	<b>19,759</b>	<b>395</b>	<b>449</b>	<b>844</b>
Wete	1,712	1,393	3,105	65	42	107
Micheweni	1,128	1,172	2,300	33	49	82
Chakechake	1,731	1,797	3,528	95	121	216
Mkoani	888	1,219	2,107	66	48	114
<b>Jumla Pemba</b>	<b>5,459</b>	<b>5,581</b>	<b>11,040</b>	<b>259</b>	<b>260</b>	<b>519</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>15,935</b>	<b>14,864</b>	<b>30,799</b>	<b>654</b>	<b>709</b>	<b>1,363</b>

**KIAMBATISHO NAMBA 9b: NYARAKA ZILIZOSAJILIWA**

<b>AINA YA NYARAKA</b>	<b>IDADI YA USAJILI</b>
A-1 (REHANI)	30
A-2 (MAUZO/URITHI)	561
A-3 (WAKFU,HIBA, KIAPO N.K)	617
A-4 (KUFUTA REHANI)	14
<b>JUMLA</b>	<b>1222</b>

**Kiambatisho Nam. 10a : Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji 2008**

<b>KIKUNDI</b>	<b>IDADI</b>
a) Ahlu Daawa	256
b) Alharamayn	83
c) Hajj Caravan & Firdaus	157
d) Jumuiya ya Istiqama	364
e) Khidmat Islamiyya	154
f) Ujumbe wa Naibu Waziri Kiongozi	4
g) ZAHATA	91
g) ZIHATA	200
i) Kamisheni ya Wakfu (02)	2
<b>Jumla</b>	<b>1311</b>

---

**Kiambatisho Nam 10b: Jumuiya zilizoombewa Msamaha wa Ushuru**

1. Jumuiya ya Muzdalifa Islamic Charitable Organization
2. Istiqama
3. Wakfu wa Mazrui
4. Al –Noor Charitable Agency na
5. Jumuiya ya Omar Bin Khatab Technical Center.

**KIAMBATISHO 11a: MISWADA ILIYOANDALIWA NA AFISI YA MWANASHERIA MKUU  
WA SERIKALI:**

Mswada wa Sheria ya Makisio ya Mwaka 2007/2008.
Mswada wa Sheria ya Fedha ya 2008 (Usimamizi wa Mapato ya Umma) 2007.
Mswada wa Sheria ya kodi ya Majengo, 2008
Mswada wa Sheria ya kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serikali 2008
Mswada wa sheria ya (Marekebisho) ya Mfuko wa Bara bara Zanzibar, 2008
Mswada wa kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ya 2008
Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini ya mwaka 2009
Mswada wa Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ya 2008
Mswada wa Sheria ya Sensa na Maonesho ya Filamu;

**KIAMBATISHO 11b: KANUNI ZA AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Sheria ndogo za maji (marekebisho) za mwaka 2008

Sheria ndogo za kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki za mwaka 2008

Sheria ndogo za usafiri wa barabara (marekebisho ya usajili na leseni za vyombo vya moto za mwaka 2008

Emblem regulations za mwaka 2008

Kanuni za usimamizi na utunzaji wa Magofu na mambo ya Kale za mwaka 2008

Kanuni za Pencheni za mwaka 2009

Kanuni za Usalama wa Vyombo za mwaka 2008

Kanuni za bidhaa madawa ya hospitali, mitishamba, na sumu

Kanuni za Mfuko wa Maendeleo ya Misititu (Marekebisho) za 2009

Kanuni za Kodi ya Ardhi (Marekebisho) za mwaka 2009

Kanuni za Stamp Duty (Registration of Hawkers) za mwaka 2009

Kanuni za Kodi ya Ongezeko la Thamani 'VAT' za mwaka 2009

Uanzishwaji wa Baraza la Biashara la Zanzibar

**Kiambatisho 12 a: Idadi ya wafanyakazi wa Wizara**

Idara/Taasisi	Wanaume		Wanawake		Jumla
	Cheti au chini	Diploma au zaidi	Cheti	Diploma au zaidi	
Afisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu	62	44	33	29	<b>168</b>
Mahakama	155	42	94	9	<b>300</b>
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	16	9	8	9	<b>42</b>
Afisi Kuu Pemba (KUB)	18	4	17	2	<b>41</b>
Idara ya Mipango na Sera	23	7	23	10	<b>63</b>
Idara ya Mufti wa Zanzibar	17	10	12	3	<b>42</b>
Idara ya Kuratibu Utawala Bora	2	8	6	4	<b>20</b>
Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi		2	3		<b>5</b>
Afisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali	29	13	21	7	<b>70</b>
Jumuiya ya Hakimiliki	1	1	1	4	<b>7</b>
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	12	22	6	12	<b>52</b>
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	51	14	29	3	<b>97</b>
Likizo bila Malipo		1		2	<b>3</b>
<b>Jumla</b>	<b>386</b>	<b>177</b>	<b>253</b>	<b>94</b>	<b>910</b>
<b>Asilimia</b>	<b>42%</b>	<b>19%</b>	<b>28%</b>	<b>10%</b>	<b>30%</b>

### Kiambatisho 12b: Idadi ya wafanyakazi Unguja na Pemba

Idara/Taasisi	Unguja		Pemba		Jumla
	W/me	W/ke	W/me	W/ke	
Afisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu	70	53	36	9	<b>168</b>
Mahakama	137	66	67	30	<b>300</b>
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	25	17	-	-	<b>42</b>
Afisi Kuu Pemba (KUB)	-	-	22	19	<b>41</b>
Idara ya Mipango na Sera	33	30	-	-	<b>63</b>
Idara ya Mufti wa Zanzibar	22	13	5	2	<b>42</b>
Idara ya Kuratibu Utawala Bora	9	8	1	2	<b>20</b>
Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi	2	3	-	-	<b>5</b>
Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali	31	23	11	5	<b>70</b>
Jumuiya ya Hakimiliki	1	5	1	-	<b>7</b>
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	29	16	6	1	<b>52</b>
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	41	20	24	12	<b>97</b>
Likizo bila Malipo	1	2			<b>3</b>
<b>Jumla</b>	<b>401</b>	<b>256</b>	<b>173</b>	<b>80</b>	<b>910</b>

**Kiambatisho 12c: Ajira Mpya**

<b>Idara/Taasisi</b>	<b>Wanaume</b>	<b>Wanawake</b>	<b>Jumla</b>
Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu	5	5	<b>10</b>
Jumuiya ya Hakimiliki	1	2	<b>3</b>
Mahakama		2	<b>2</b>
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	2	5	<b>7</b>
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana		1	<b>1</b>
<b>Jumla</b>	<b>8</b>	<b>15</b>	<b>23</b>